JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU

SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MWADUI

S.L.P 32

MWADUI

6/12/2022

Barua pepe mwaduitechnical@gmail.com

Kumb.Na.MTSS/FI J /2023

Kwa -------------------------------------------------

-------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE ( JOINING INSTRUCTIONS) KIDATO CHA KWANZA 2023 SHULE YA SEKONDARI MWADUI UFUNDI**

**1.0** Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na Shule hii katika kidato cha kwanza **2023,KARIBU SANA MWADUI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**.Shule hii ni ya mchepuo wa Ufundi na ni mchanganyiko ( wavulana na wasichana ).Nina imani kubwa kwamba utafurahia kusoma katika shule hii.

Shule ya sekondari ya ufundi Mwadui ipo mkoa wa Shinyanga wilaya ya Kishapu, ndani ya Mgodi wa Almasi Mwadui , ¼ km kutoka Geti kuu la kuingilia Mgodini na ipo umbali wa 3km kutoka Barabara kuu ya Shinyanga -Mwanza. Ukisafiri kwa Mabasi ya kutoka mikoani,unaelekezwa kuteremka katika Standi ya mabasi ya Maganzo ambapo utachukua usafiri wa Bajaji/Pikipiki hadi Shuleni kwa nauli isiyozidi Tshs 2,000.

**2.0 SARE ZA SHULE WASICHANA**

.Siketi 2 rangi ya Samawati ( Dark blue ),kwa wasichana wa kiislam wanaruhusiwa kuvaa Hijab
.Blauzi/Shati nyeupe mikono mifupi jozi 2
.Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba ,siyo buti na visiwe na visigino virefu.
.Soksi nyeupe
.Sweta rangi ya Blue ambalo mzazi atalinunua hukohuko
.Tshirt kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa ambazo zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 12,000
**NB**:Siketi zinatakiwa kushonwa katika mtindo wa Rinda box ,ziwe ndefu kukaribia kugusa viatu.

**2.1 SARE WAVULANA**

.Suruali rangi ya samawati ( Dark blue ) jozi 2
.Shati nyeupe mikono mifupi jozi 2
.Viatu vyeusi vyenye kamba ,siyo buti na visiwe na visigino virefu.
.Soksi rangi nyeusi
.Mkanda mweusi wa ngozi wenye kifungio cha kawaida
.Sweta rangi ya Blue ambalo mzazi atalinunua huko huko.
.Tshirt kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa ambazo zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 12,000.
NB.Suruali chini ziwe na upana wa inchi 17 au 18,mbele iwe na rinda 2 ( Celebration ) kila upande na mifuko 2 ya Cross na nyuma iwe na mfuko 1.Ni marufuku kwa mwanafunzi kushona na kuvaa nguo zilizobana ( Vimodo ),hivyo hazitakubalika na unaweza kuingia hasara ya kushona upya.

**3.0 MAHITAJI BINAFISI YA MWANAFUNZI**

Mzazi unatakiwa kumkamilishia mwanao mahitaji yafuatayo:
( i ) Daftari zenye ukubwa wa wastani au Counter book 14 au zaidi
( ii ) Kalamu za wino blue au nyeusi 2 au zaidi
( iii ) Kramu za risasi 2
( iv ) Rula,Kifutio na Mathematical set 1.
( v ) Scientific Calculator 1

**3.1 MAHITAJI YA JUMLA**

( i ) Aje na mfagio wa Chelewa mmoja ( 1 ) wenye mti kwa usafi wa mazingira ya Shule

( ii ) Aje na ufagio wa ndani 1 ( Soft broom ) kwa usafi wa ndani

( iii ) Aje na Ream paper 1 kwa mwaka kwa uzalishaji na ufanyikaji wa Mitihani na mazoezi.

**4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa Sheria ya Elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyolrekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu ,Sayansi na Technolojia ,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

( a ) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

( b ) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

( c ) Kushiriki kwa makini kufanya maadalio ya jioni ( preparation studies)

( d ) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

( e ) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

( f ) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya Shule

( g ) Kuvaa Sare ya Shule wakati wote ukiwa mazingira ya shule

( h ) Kuzingatia ratiba ya Shule

( I ) Kutunza mali za Umma/Shule

**5.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO**

( a ) Wizi
( b ) Uasherati na Ushoga

( c ) Ubakaji

( d ) Ulevi,matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi,Cocaine,Mirungi nk,
( e ) Kupigana au kupiga
( f ) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
( g ) Kudharau Bendera ya Taifa
( h ) Kuwa mjamzito/Kupata Mimba
( I ) Kuoa au Kuolewa
( j ) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
( k ) Kukataa adhabu kutokana na makosa uliyotenda
(l ) Kumiliki na kutumia Simu mazingira ya Shule na Bweni

**6.0 MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KULETWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

( a ) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospital ya serikali.Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.
( b ) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
( c ) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
Unatakiwa kusoma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
NB:Suala la mwanafunzi kumiliki na kutumia **SIMU** Shuleni halikubaliki na halitavumiliwa.Mwanafunzi akikamatwa anamiliki na kutumia **SIMU** atafukuzwa Shule mara moja.Mzazi unashauriwa kukaa na mwanao umueleweshe mapema juu ya jambo hilo.

**MAZINGIRA YA SHULE KWA TAALUMA NI MAZURI KWA ANAYEJITUMA KUSOMA.**
**KARIBU SANA UPATE ELIMU BORA**

____________________________

**MKUU WA SHULE**

**MWADUI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 32**
**MWADUI**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**PART A**

To:Medical Officer
---------------------------------------------
-----------------------------------------------

RE: MR/MISS------------------------------------------------------------------------
Name in full

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for full time School course.The examination should include the following categories I – III each category or sub –category of which will render the applicant in –eligible in case of defect. Pregnancy category IV will also render a girl candidate ineligible for the course.

I.( a ) Eye sight
( b ) Hearing
( c ) Limbs
( d ) Speech
( e ) Venereal Disease
( f ) Leprosy
( g ) Epilepsy
II. Neuroses
III. Other serious Diseases
IV. Pregnancy

____________________________
**HEADMASTER**

**PART B**
**MEDICAL CERTIFICATION**

To be completed by Government Medical Officer

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit /unfit and mentally fit/unfit for full time school course.

I.( a ) Eye Sight------------------------------
( b ) Hearing----------------------------------
( c ) Limbs ------------------------------------
( d ) Speech-----------------------------------
( e ) Venereal Diseases ------------------
( f ) Leprosy -----------------------------
( g ) Epilepsy----------------------------
II.Neuroses
III.Other serious Diseases
IV.Pregnancy

Signature------------------------------ Station------------------------
Designation---------------------------- Date ---------------------------

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MWADUI**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI ( Ijazwe na Mwanafunzi** )

(i ) Majina kamili ya Mwanafunzi-------------------------------------------------------------
NB:Majina lazima yawe aliyofanyia Mtihani darasa la Saba.

Shule atokayo------------------------------------------------------------
( ii ) Tarehe ya kuzaliwa--------------------------- Wilaya-------------------------Mkoa----------------------
( iii ) Dini -------------------------------------- Dhehebu-----------------------------------------
( iv ) Jina la mzazi/Mlezi --------------------------------------------------------------------------------
( v ) Kabila---------------------------------------------
( vi ) Namba za Simu za mzazi/mlezi -----------------------------------------------
( vii ) Kzai ya mzazi /mlezi-----------------------------------------------------------------------

**SHEMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI**
Mimi---------------------------------------------------------------------------- ambaye ni mzazi wa mwanafunzi --------------------------------------------------------------- ninakiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo yaliyotolewa kuhusu nidhamu za mwanafunzi.Naahidi kutoa ushirikiano wa kutosha katika kusimamia nidhamu ya mwanangu kwa faida ya taaluma yake.

Jina la mzazi /mlezi--------------------------------------------------------------

Saini----------------------------------------Tarehe----------------------------------